



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JULAI, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 AGOSTI, 2023

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JULAI, 2023

Katika dekad hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuwa imeimarika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii iliendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu na hivyo kusababisha kuendelea kwa vipindi vya upepo mkali katika baadhi ya maeneo ya nchi. Joto la bahari katika eneo la Kusini Mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), Magharibi mwa bahari ya Hindi na kati ya Ikweta mwa bahari ya Pasifiki lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Kwa upande mwingine, joto la bahari Mashariki mwa bahari ya Hindi lilikua la chini kidogo ya wastani. Hali hizi zilikuwa na mchango kidogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JULAI, 2023

Katika kipindi hiki, maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu na yenye hali ya ubaridi. Hata hivyo, vipindi vifupi vya mvua nyepesi viliripotiwa katika maeneo ya miinuko ya Nyanda za juu kaskazini-mashariki na ukanda wa pwani vikiambatana na vipindi vya upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 AGOSTI, 2023

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 AGOSTI, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika. Hali hii inatazamiwa kuendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo

mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu na na hivyo kuleta mchango katika kusukuma hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la Kusini Mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), Magharibi mwa bahari ya Hindi na kati ya Ikweta mwa bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani. Kwa upande mwingine, joto la bahari Mashariki mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa chini kidogo ya wastani. Hali hizi kwa ujumla zinatarajiwa kuwa na mchango kidogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 AGOSTI, 2023

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na yenye hali ya ubaridi. Hata hivyo, vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo ya miinuko vinatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vifupi vya mvua nyepesi yenye upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa baharini vinatarajiwa.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi pamoja na vipindi vifupi vya mvua nyepesi yenye upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa baharini vinatarajiwa.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA